

**Taarifa ya Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa Kuhusu Wanafunzi wa Kitanzania Waliodhalilishwa Bangalore – India**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa nimetoa taarifa ya awali kuhusu matukio huko Bangalore katika Jimbo la Karnataka - India, ambako wanafunzi wa Kitanzania walipigwa na mmoja wao msichana alidhalilishwa kwa kuvuliwa nguo na kutembezwa hadharani barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tulizozipata, zinathibitisha kwamba kweli kitendo hicho kilitokea na kilifuatia uendeshaji mbaya wa gari na mwanafunzi kutoka Sudan ambaye aligonga pikipiki tatu na baada ya hapo akamgonga mama wa Kihindi aliyefariki pale pale barabarani.

Baada ya tukio hilo, huyo mwanafunzi wa Sudan alikimbia. Wananchi wa India waliokuwa jirani walichoma gari lake na punde kidogo gari lingine lilifuata likiwa na wanafunzi wanne wa Tanzania, mmoja msichana na watatu wavulana. Walilisimamisha gari lile na kuwavuta wale wanafunzi nje na wakamchukua yule msichana na kumvua nguo na kuanza kumtembeza barabarani uchi. Wale wavulana walipigwa na gari lao lilichomwa moto. Katika gari ile walikuwa na simu zao na *documents* zao mbalimbali nazo ziliteketea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo polisi walikuja lakini hawakutoa ushirikiano wa kutosha. Hata hivyo, waliweza kuwapeleka wale wanafunzi hospitali na kule hospitali walionekana wana majeraha makubwa, wakatibiwa lakini ikabidi waondoke kwa sababu walikuwa hawana pesa za kutosha kugharamia matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, Ubalози wetu India, kama nilivyosema jana, uliandika Dokezo la Kidiplomasia kwa Serikali ya India kulaani kitendo hicho na kuitaka Serikali ya India ichukue hatua za kisheria na za haraka kupeleleza kufuatia matukio hayo. Kwa upande wetu kama Wizara, jana tulimuita Balozi wa India aliyepo hapa nchini na kumueleza jinsi Serikali na wananchi wa Tanzania walivyofadhaika na kuchukizwa na kitendo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi alituambia kwamba na yeye amejulishwa na Serikali yake kuhusiana na suala hilo na Serikali ya India na Waziri mwenyewe wa Mambo ya Nchi za Nje wa India alitoa taarifa rasmi kule New Delhi, kwanza kuomba radhi kwa Tanzania na Watanzania waliopo India kwa kitendo hicho kilichotokea. Pia akaagiza Serikali yake ichukue

hatua za kisheria na kupeleleza na kuwakamata wale waliohusika na wote sasa wamekamatwa na wamepelekwa mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali ya India iliagiza kwamba wanafunzi wa Tanzania wapewe ulinzi maalum kule wanakoishi na waweze kusindikizwa wanapokwenda masomoni au madarasani. Tatu, Serikali ya India ilimtaka Balozi wetu afuatane na Maafisa Waandamizi wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya India kwenda Bangalore ili kukutana na wanafunzi wa Tanzania na wengine wa Afrika lakini pia kukutana na jumuiya ya maeneo ambayo Watanzania wanaishi kwa sababu vitendo hivi vinaashiria ubaguzi na kuweka mahusiano mazuri kati ya wanafunzi na wenyeji katika maeneo ya mji huo na hasa maeneo yale ambapo wanaishi. Hilo limetokea, Balozi wetu amefuatana na maafisa hao kwenda Bangalore na mikutano hiyo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana pia nilieleza kwamba kuna mwanafunzi mmoja ambaye alifariki karibu na maeneo hayo hayo. Taarifa za awali zilikuwa zinatatanisha, tukadhani kifo hicho kilitokana na tukio hilo la kuvamiwa wanafunzi wetu lakini si kweli.

Mwanafunzi huyo Mtanzania, alikuwa anaendesha pikipiki bila kofia, akagonga nguzo ya taa na kufariki pale pale. Ubalozi wetu unashughulikia mazishi na mwili wake utarudishwa Tanzania mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo taarifa ambayo ilitokana na swali la jana nimeona ni vema nilijulishe Bunge lako Tukufu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*